BOARD OF DIRECTORS
Osvaldo F. Avila, Chairperson • Ashley Carson Cottingham, Vice Chairperson
Danielle Bethell • Satya Chandragiri • Marty Heyen
Karina Guzmán Ortiz • María Hinojos Pressey
PO Box 12024, Salem, Oregon 97309-0024
503-399-3001

Christy Perry, Superintendent

**AJENDA**
**MKUTANO WA BODI**
**JULAI 27, 2021**
**Saa 11 jioni Kikao cha watendaji (Kikao kisicho cha umma)**
**Saa 12 jioni Kikao cha kazi (Kikao cha umma)**
Kituo cha huduma ya msaada 2575 Commercial Street SE Salem OR 97302. Chumba cha mkutano wa bodi kitakuwa wazi kwa umma na wafanyakazi walioteuliwa chenye uwezo wa kukaa watu 65

**Upatikanaji mubashara kwa umma**
English: https://youtu.be/6HCnfAJmxAE
Spanish: https://youtu.be/IeAjhopezAU
Mkutano pia utarushwa kupitia CC: Media channel 21

1. **KUFUNGUA** — Mwenyekiti
   a. Mahudhurio ya Bodi

2. **KIKAO CHA WATENDAJI** — Mwenyekiti
   Bodi watakutana kwenye kikao cha watendaji chini ya Kanuni Zilizorekebishwa za Oregon:
   a. ORS 192.660(2)(d) kufanya mazungumzo na watu walioteuliwa kuendelea na mazungumzo ya kazi
   b. ORS 192.660(2)(f) kuzingatia habari au rekodi ambazo haziruhusiwi na sheria kutoka kwa ukaguzi wa umma
   Wawakilishi wa vyombo vya habari wanaruhusiwa kurudhuria kikao cha watendaji isipokuwa, vikao vinavyohusisha kufukuzwa. Washiriki wengine hawarusiwi kwenye kikao cha watendaji na wanaombwa kutoka katika eneo la mkutano. Wawakilishi wa vyombo vya habari mahususi wanaombwa kutokutoa taarifa kuhusu yeyote wakati wa vikao cha utendaji, isipokuwa kuelezea mada ya jumla ya kipindi kama ilivyoorodheshwa kwenye ajenda. Hauruhusiwi kurekodi kikao cha watendaji bila idhini ya wazi kutoka kwa bodi

3. **KUUNGANA TENA** Saa 12 Jioni — Mwenyekiti
   a. Utambuzi wa ardhi
   b. Ahadi ya Utii
   c. Muundo wa Ajenda

4. **MAONI KWA UMMA:** ***Vitu vya kikao cha kazi tu*** — Mwenyekiti
   Bodi itasikia maoni ya umma kwa **saa moja** kwenye **vitu vya kikao cha kazi tu** kwa kuhudhuria, au kupiga simu, na kutuma kwa njia ya maandishi. Kila mshiriki atapewa dakika tatu, na nyongeza ya dakika tatu kutafsiri kwa lugha ya Kiingereza kama itahitajika. Kiungo cha kujiandikisha ili kutoa maoni kitafunguliwa mara tu ajenda zinapo bandikwa siku ya Ijumaa Julai 23, mchana na zitafungwa Jumatatu Julai 26 mchana. Tafadhali bonyeza hapa click here kwa maelekezo na kujiandikisha kwa maoni. Kutakuwa na fomu ya kujaza kwenye chumba cha mkutano kwa maoni ila itakuwa ni kuwahi kujiandikisha na muda unavyoruhusu. **Kujiandikisha kupitia kwenye kiungo ndiyo muafaka kwa maoni yote ya umma (kuwepo pale, kupiga simu au kuandika.**

   Bodi itapokea maoni kwa maandishi kabla ya mkutano na bodi na itasikiliza muhtasari wa maoni wakati wa mkutano. Muhtasari wa maoni kwa maandishi utaweka kwenye mtandao kama nyenzo za ziada kwa mkutano mwingine siku ya kazi.

5. **KIKAO CHA KAZI**
   a. *Pendekezo la maoni ya umma kwa Mikutano ya Bodi ya Umma — Mwenyekiti
   b. *Mipango ya Ushiriki katika Jamii Kurudi Shuleni kipindi cha Fall — Superintendent

6. **KUAHIRISHWA** — Mwenyekiti

*Taarifa za Msaada Zimejumuishwa

# PENDEKEZO LA MAONI YA UMMA KWA MIKUTANO YA BODI YA UMMA

## Usuli/Majadiliano

Wakati bodi ya shule inaporudisha mikutano uso kwa uso, bodi ya kurugenzi imejidhatiti kusikia kutoka kwa umma wakati wa kipindi cha bodi ya mikutano kupitia mchakato wa maoni kwa umma.

Siku ya Julai 13, 2021 bodi ya shule ilisikia pendekezo kwenye maoni ya umma wakati bodi ikirudi kwenye mikutano ya uso kwa uso. Bodi ilijadili pendekezo wakati wa mkutano. Uongozi wa bodi ulipokea taarifa kutoka kwenye bodi, na kufanyia mabadiliko mapendekezo na kukubali maoni ya umma kuhusiana na mapendekezo.

## Ushauri/Hatua ya Bodi

Hakuna hatua iliyochukuliwa kwenye hiki kipengele. Baada ya kupitia maoni ya umma, uongozi wa bodi utafanya maamuzi kupitia mchakato wa maoni ya umma kwenye mkutano wa bodi mwezi Agosti. Mchakato wa maoni ya umma utakuwa unawekwa kwenye ajenda na kwenye tuvuti ya ukurasa wa bodi ya shule.

**PENDEKEZO LA MAONI YA UMMA KWA MIKUTANO YA BODI YA UMMA**

Bodi inataka kusikia maoni kutoka kwenye jamii kuhusiana na kazi ya bodi na maamuzi, wakati muda huo huo ufanisi unavyofanywa kwenye kazi ya bodi. *Bodi imejidhatiti kutoa muda wa kutosha katika kufanya maamuzi ili umma uweze kutoa maoni kwa kiwango kikubwa iwezekanayo. Bodi pia imejidhatiti kutafuta njia nje ya maoni ya umma katika mchakato wa ushiriki kwenye jamii*.

Kufuatia haya malengo, utaratibu wa maoni ya umma utakuwa kama ifuatavyo:

- Maoni ya umma yatakuwa wazi mara ajenda zitakapotolewa siku ya Ijumaa kabla ya mkutano wa bodi na yatafungwa saa 10 jioni siku ya Jumatatu. Wilaya itafanya kila jitahada kuhakikisha kuwa ajenda zinawekwa ifikapo mchana wa Ijumaa na siyo zaidi ya saa 11 jioni.
- Dakika 30 mpaka 60 jumla ya muda kwa ajili ya maoni ya umma; kila msemaji ataruhusiwa dakika 3 na zitagawanywa sawa kati ya mpiga simu na yule aliyehudhuria kutoa maoni.
- Kwa kufuata busara za mwenyekiti wa bodi, mwenyekiti anaweza kuongeza muda wa mkutano kwa ajili ya maoni kwa umma kuhusiana na mada maalumu.
- Aliyehudhuria au anayepiga simu lazima aweze kusimamia mada maalumu kwa "vitendo" na "kusoma" vitu vilivyoorodheshwa kwenye ajenda ili bodi isikie maoni juu ya vitu hivi kabla ya kufanya uamuzi.
- Ili kuwa na usawa na haki, watu watajiandikisha kutoa maoni waliohudhuria au kwa kupiga simu watachaguliwa kupitia makundi* orodha ya fomu ya kujiandikisha na kufuata orodha iliyoandikishwa.
- Wale watakao kuwa wanapiga simu watapatiwa namba ya kupiga wakati wa mkutano.
- Kujiandikisha siyo kwamba unahakikishiwa nafasi ili utoe maoni (Hii inategemea na watu wangapi wamejiandikisha, makundi na muda uliopo)
- Maoni ya kuandika yanakaribishwa kwenye ajenda na yale yasiyokuwa kwenye ajenda lakini yananufaisha umma.
- Maoni ya kuandika ya sizidi herufi 2000, ambayo ni sawa na maneno 250.
- Maoni ya kuandika yatapelekwa kwa bodi kabla ya mkutano na kufupishwa ndani ya chumba cha bodi wakati wa mkutano.

*Makundi yanajumuisha yafuatayo:

- Wanafunzi
- Wazazi
- Mwanajamii mmoja mmoja (siyo sehemu ya kundi)
- Kundi/Shirika – (jina la kundi)
- Wafanyakazi wa Wilaya
- Kwa niaba ya SKEA
- Kwa niaba ya ASKESP

# MIPANGO YA USHIRIKI KATIKA JAMII KURUDI SHULENI KIPINDI CHA FALL

## Usuli/Majadiliano

Shule za umma Za Salem-Keizer zimejidhatiti kuwa na malengo ya kufundisha siku tano uso kwa uso kwa wanafunzi wote wa wilaya. SKPS imejenga uhusiano kupitia Mamlaka ya Afya na Wilaya ya SKPS pamoja na Afya ya Umma kwa kata za Polk na Marion. Wilaya yetu ilianzisha mazoea ya usalama wakati wa mwaka wa shule 2020-21 pale tulipohamia kusoma uso kwa uso kwa wanafunzi wachache na kusoma kwa njia ya mtandao.

Idara ya Elimu ya Oregon kwenye utayari wa shule kusoma salama umehama kutoka kwenye ngazi ya jimbo kwenda kwenye mahitaji ya ushauri, kurudisha maamuzi tena kwenye ngazi ya wilaya za shule.

SKPS inapanga mfululizo wa ushiriki katika jamii kurudi mashuleni kwa mwaka wa shule 2021-22 na inaangalia taarifa ya mrisho nyuma kwa kurudi shuleni.

## Ushauri/Hatua ya Bodi

Hakuna hatua inayohitajika kwenye kipengele hiki. Inaletwa kama mada ya kikao cha kazi kupata maoni ya umma kwenye ushiriki wa mpango na kuruhusu bodi kutoa maoni kwenye mipango. Wafanyakazi wa wilaya wataleta mpango uliopendekezwa na kushiriki mada kutoka kwa jamii wakati wa mkutano wa bodi mwezi Agosti.

**MIPANGO NA MAWASILIANO WAKATI WA KURUDI MASHULENI KWA MWAKA 2021-22**

**KUSUDI:** KUTOA FURSA KWA WAZAZI NA WANAFUNZI KATIKA KUTOA MAWAZO YAO KWENYE MIPANGO YA KURUDI SHULENI

Kama mipango inavyozidi kuendelea ya kurudi shuleni kipindi cha fall, SKPS inapanga mfululizo wa vipindi vya ushiriki kwa familia kwa mwaka wa kurudi shule 2021-22. Tunaamini kwamba, kwa kuweka kipaumbele kwenye sauti na maoni kutoka kwa wanafunzi na wazazi. Lengo letu ni kurudi kufundisha siku tano uso kwa uso na kukidhi mahitaji katika jamii yetu huku tukihakikisha usalama na ustawi wa wanafunzi wanaohudhuria shule zetu.

**Jitihada za ushiriki wa wanafunzi na wazazi zinalenga kusaidia wilaya kupanga na kwa kuelewa:**

- Jinsi gani SKPS itasaidia familia kujiandaa kurudi kusoma uso kwa uso siku tano kwa wiki?
- Familia ina wasiwasi gani kuhusu kurudi shule?
- Ni mfumo gani wilaya inaweza kuweka ili kumsaidia mwanafunzi katika mchakato wa kurudi shule kipindi cha fall?
- Ni mahitaji gani kwenye jamii yetu ya tofauti na tunavyoendelea kuangalia kwenye lensi ya usawa?

**Njia ya Ushiriki na Muda:**
Julai 26 – Agosti 11

- **Mawasiliano:** Matangazo ya vipindi cha ushiriki, utafiti, na njia mbili za fursa ya mrisho nyuma. Kwa kutumia teknolojia kama vile ParentSquare, ambayo inatoa huduma ya simu kwa sauti, email, na ujumbe wa maneno. Kutumia jukwaa la mtandao wa kijamii.
- **Video kutoka kwa Superintendent:** Video ya ushiriki kwenye kurudi shuleni ya kutoka kwa Superintendent Perry, iliyotafsiliwa kwa lugha mbalimbali
- **Watumiaji barua:** Matukio mubashara ya kuwaalika familia
- **Mikutano ya dhahiri:** Kuongea mubashara na Superintendent Perry na/au timu ya uongozi, kwenye mpangalio halisi kukusanya taarifa ili kusaidia mahitaji ya familia kwa mwaka wa shule 2021-22. Tutakuwa na vipindi kwa Kiingereza na familia ambazo Kiingereza siyo lugha yao kwanza (Marshallese, Kiarabu, Kispanish, Chuukese, Swahili na Kirusi)
    - **Ratiba ya muda Agosti 4 & 6, Saa 12 jioni – Saa 1 usiku (6pm -7pm)**

      **LENGO:** KUSHIRIKISHANA KWENYE TAARIFA KUHUSU MIPANGO YA MWISHO YA KURUDI SHULENI

Agosti 16 – Septemba 10

- **Mikutano ya Dhahiri:** Ratiba ya muda.
    - Shule ya msingi – Wiki ya Agosti16
    - Shule za sekondari – Wiki ya Agosti 23
- **Sasisho za Mawasiliano:** Muendeleo wa sasisho na mawasiliano kutoka shule kwenda kwa familia kuhusu usalama, kujifunza na ustawi.
- **Watumiaji barua:** Vipindi vya kurudi shuleni na familia
- **Taarifa za Video kutoka kwa Superintendent:** Sasisho na ujumbe kutoka kwa Superintended Perry kwa wakati unaofaa.
- **Sehemu ya kupata rasilimali.** Maswali na majibu ya mara kwa mara kwenye mtandao na tuvuti ya shule na wilaya.